Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 81 No. 226 | MUHAR - SAFAR 1443AH | SEPTEMBA 2021 | IKHA 1400 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na siri za mbingu na ardhi ni za Mwenyezi Mungu, na habari yote itarudishwa Kwake. Basi Mwabudu Yeye na kumtegemea. Na Mola wako Haghafiliki na yale mnayoyatenda. (Huud 11:124)

Ni Heshima na Fahari kwa Tanzania

• Tuzo ya Fasihi ya Nobel 2021 yatunukiwa kwa Abdulrazak Gurnah

• Rais Samia, Rais Mwinyi watuma salamu za pongezi



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhajj Dr Hussein Mwinyi



Abdulrazak Gurnah, mshindi wa tuzo ya Nobel kwenye fasihi 2021



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan

Makala uk 2

Maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad saw

Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a. Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa as

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

KUIKUBALI ISLAM KWA WENYEJI WA MADINA

Katika kipindi hiki Mtume s.a.w. alikuwa mara kwa mara akipokea habari toka kwa Mwenyezi Mungu kuwa wakati wako wa kufanya Hijra (kuhama) unakuja na ilikuwa imeshafunuliwa kwake kuwa sehemu atakayohamia ni mji wenye visima na wenye mashamba ya mitende pia. Mwanzoni alidhani kwamba labda sehemu hiyo atakayohamia ilikuwa ni Yamama, lakini wazo hili likaondolewa haraka moyoni mwake naye akawa anasubiri kwamba ule mji uliokadiriwa sawa na bishara ya Mwenyezi Mungu, wenyewe utajitolea kuwa mlezi wa Islam.



Ndani ya muda huo huo zikaja siku za Hija. Watu kutoka pembe zote nne za Uarabuni wakaanza kujumuika Makka kwa ajili ya kuhiji. Naye Muhammad s.a.w., sawa na desturi yake, popote pale alipowaona watu wamesimama, basi alikuwa akiwaendea na kuanza kuwapa mawaidha ya Umoja wa Mwenyezi Mungu na kuwapa habari njema za ufalme wa Mwenyezi Mungu na kuwapa nasaha za kuepukana na dhulma, matendo mabaya, ufisadi na utukutu.

Baadhi ya watu walikuwa wakiyasikiliza maneno yake kwa mshangao na kisha kuondoka zao. Baadhi wakawa wakimsikiliza na watu wa Makka wakawa wakija na kuwaondoa. wengine waliokuwa wameshayasikia maneno ya watu wa Makka walikuwa wakimcheka na kujiondokea.

Alikuwa akiranda randa katika hali hii hii kwenye bonde la Mina alipoonekana na watu sita au saba hivi waliokuwa wenyeji wa Madina. Akawauliza: 'Ninyi mwatokana na kabila lipi?' Wakamjibu: 'Twatokana na kabila la Khazraj.' Akawauliza tena: 'Ni kabila lile lililowekeana mkataba na Wayahudi?' Wakajibu: 'Ndiyo.' Akawauliza: 'Je mwaweza kuketi kwa muda na kuyasikiliza maneno yangu?' Watu hao wakalikubali ombi lake kwani tayari walikuwa wameshapata habari zake na hivyo walikuwa na shauku moyoni ya kuusikiliza ujumbe

Endelea uk. 3

Askari wawili waikomboa Daluni uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

MFANO MWEMA

Hakuna kiongozi yeyote wa kidini au wa kisiasa ambaye maisha yake ni bayana na yamewekwa kweupe kama yale ya Mbora wa daraja, Rehema kwa walimwengu, Mtukufu Muhammad rehema za Allah na amani ziwe juu yake. Jitahidi kumsoma Nabii Isa as, Budha as, Zoroaster, Krishna, kwa upande wa dini au George Washington, Abrahama Lincoln, Mahatma Gandhi, Gamal Abdel Nasser, Wiston Churchill, Kwame Nkurumah, Vladmir Lenin, Mao Tse Tung, Sekou Toure, kwa upande wa siasa lakini bado kuna mengi yasiyojulikana juu yao. Lakini sio hivyo kwa Mbora wa viumbe wote na hiyo ni kwa sababu ya sababu zifuatazo.

Mtukufu Mtume*saw* tofauti na manabii wote wengine wa kabla yake ni yeye aliyetumwa kwa binadamu wote na ametumwa kuwa mfano bora katika kila kipengele cha maisha ya mwanadamu. Hulka yake imeelezwa na Allah, "kwa hakika mna mfano mwema kwa Mtume wa Allah". Hili ni jukumu zito ambalo alitakiwa alionyeshe kwa walimwengu ili waweze kufuata na kuiga mfano huo. Waarabu wamejaaliwa ubongo mkali na uwezo mkubwa wa kukumbuka mambo. Kwa miaka mingi walikuwa na utamaduni wa kurithishana historia ya kizazi kimoja hadi kingine. Historia ya ukoo ilifahamika, iliheshimika, na kutunzwa kwa ghera kubwa na jamii. ilikuwa ni fahari kubwa kwa mwanaukoo kusimama na kujinasibu. Wako watu maalum ambao walipewa jukumu hili. Elimu hiyo muhimu iliitwa *ilmun nasab*. Washairi wa Kiarabu waliandika beti nyingi za kihistoria na zimewezwa kukumbukwa kwa ghaibu. Chemchem nyingine ya kumfahamu Mtukufu Mtume*saw* tumeelezwa na Bi Aisha ra nayo ni Quran Tukufu, matendo yake na hulka zake kwa ujumla ni Quran Tukufu. Ukikutana na jambo lolote katika maisha ya Mtukufu Mtume*saw* linakwenda kinyume na Quran Tukufu uwe na uhakika na utulivu kwamba hilo sio lake. Kinyume na manabii wengine ambao wafuasi wao walisema 'nenda wewe na Mola wako mpigane', wengine wakamkana mara tatu na jogoo likawika. Mtukufu Mtume Muhammad*saw* alikuwa na masahaba waliompenda sana, kila jambo lake walilitizama kwa uangalifu na kuiga, hata wakati anatawadha walikinga ili kupata baraka ya maji yale. Mapenzi yao yalifikia kusema 'tutapigana nawe kushoto na kulia, hata ukituambia tujitupe baharini hutamkuta yeyote aliyesimama'. Kwa njia hii maisha ya Mbora wa viumbe wote yameelezwa kinagaubaga na hatuna haja ya mahangaiko ya kutafuta mwongozo mahali pengine.

Kuhusu mtukufu mtume sawa tunapata maelezo alivyolala, alivyoamka katika usingizi, alivyopiga mswaki, nguo alizovaa, jinsi alivyokula na kunywa, jinsi alivyokaa na kusimama, jinsi alivyotembea. Namna alivyozungumza, alivyoamua kukaa kimya, jinsi alivyoonyesha furaha na huzuni, mwenendo wake akiwa mume wa ndani. Alitumia vipi wakati wake akiwa safarini. Namna gani alivyozungumza na watoto. Alivyowapokea wapendwa wake na waheshimiwa kutoka nje. Alivyotimiza ahadi ya urafiki na mapatano. Mwenendo wake wakati wa mapatano na amani. Namna alivyopigana katika vitalu. Alivyotekeleza wajibu wake kwa Allah na viumbe wa Allah. Jinsi alivyosikiliza maneno ya Allah na kuyaeneza. Kila tendo lake liwe dogo kiasi gani limehifadhiwa.

Kama hali halisi kumuhusu Mtukufu Mtume Muhammad*saw* ni hii tunao wajibu unaoweza kugawanywa katika sehemu tatu. Tuongeze sala ya Mtume, tuendelee kumuombea kwa nguvu zetu zote kwani mapenzi yake kwetu yalikuwa makubwa na kumuombea kwetu ni amri. Tujitahidi kusoma kuhusu maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad*saw*, yapo mengi sana ambayo yameandikwa, tuyasome, tuyazingatie na pale palipo na upotoshaji tusahihishe. Kabla ya kutenda tendo lolote tujikumbushe katika hili mtukufu Mtume Muhammad*saw* alifanyaje? Kazi hii inaonekana ni kubwa na nzito, lakini ni jambo la kutoa shukurani kwa Allah kwani amerahisisha kazi hiyo kwa kumleta mwana wa kiroho wa Mtukufu Mtume Muhammad*saw*, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad*as* ambaye ametueleza kila tunachotakiwa ili kuipata shabaha ya kuinuliwa kwa Mtukufu Mtume Muhammad*saw* Vipo vitabu vingi ameviandika ambavyo vinapatikana katika Kiswahili na Kiingereza.

Sote kwa pamoja tusome maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad*saw* kwani maisha yake ni muhimu katika historia ya binadamu kama alivyosema mwanahistoria maarufu W. M. Watt katika *Muhammad at Medina*.

Mtu anapozungumzia historia ya Muhammad na siku za mwanzo za Islam, anashangaa juu ya mafanikio yake makubwa, na isingekuwa kwa vipaji vyake vya kuona mbali, uongozi mahiri, imani thabiti kuwa Allah Amemtuma, ukurasa wenye shani katika historia ya binadamu usingeandikwa.

Ni heshima na fahari kwa Tanzania



Mahmood Hamsin Mubiru

Kwa nyakati tofauti Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhajj Dr Hussein Mwinyi wamemtumia salamu za pongezi Abdulrazak Gurnah kwa kutunukiwa tuzo kubwa kuliko zote katika uwanja wa fasihi kwa mwaka 2021.

Abdulrazzak Grunnah mzawa kindakindaki wa visiwa vya karafuu Zanzibar ameiletea heshima na fahari kubwa nchi alikozaliwa na kuliko kitovu chake – Tanzania. Yeye sasa anaungana na wana wa Afrika walioiletea bara hili sifa kwa kutunukiwa tuzo hiyo. Hao ni pamoja na Naguib Mahfudh wa Misri, Nadine Gordiner, John Maxwell Coetzee wote wa Afrika Kusini, Wole Soyinka wa Nigeria. Waandishi wengine maarufu duniani waliopokea tuzo hiyo iliyoanza kutolewa 1901 ni Ernest Hemingway, T. S. Eliot, Pablo Neruda, kwa kuwataja wachache.

Abdulrazak Gurnah alizaliwa Malindi Zanzibar tarehe 20 Disemba 1948 na kupata elimu yake ya awali kisiwani humo. Kufuatia mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964 huko Zanzibar Abdulrazak akiwa na umri wa miaka 18 aliingia Uingereza akiwa mkimbizi. Kwa bidi kubwa na kujituma aliendelea na masomo hadi kupata shahada ya uzamivu kutoka chuo cha Kent Uingereza. Mara baada ya kuhitimu alipea nafasi ya kufundisha lugha ya Kiingereza na fasihi inayoambatana na athari za ukoloni. Na mafanikio yote hayo katu hakusahau nyumbani kwao. Kwa kutumia kalamu alianza kuandika juu ya mambo mawili ambayo yanatawala katika kazi zake. Kwanza, athari za ukoloni kwa wananchi wa mwambao wa Afrika Mashariki. Na katika hili la kuzungumzia ukoloni na athari zake hayuko peke yake. Waandishi kama Chinua Achebe, Mungo Beti, Camara Laye, Ngugi wa Thiong'o, V. S. Naipaul, George Lamming, wameeleza athari za ukoloni katika kazi zao walizoandika. Jambo la pili ameeleza kinagaubaga adha wanazopata wakimbizi wanaokimbia kutoka nchi zao na jitihada za kujenga daraja ili kuzikutanisha tamaduni ili zipate kuishi pamoja kwa maelewano. Katika kazi zake zote hizo wahusika ni watu tunaowafahamu vizuri katika Afrika Mashariki. Athari za wakoloni za wagaweuwatawalenajinsi wanasiasa wanavyozidi kuweka msumari wa moto kwenye donda, zimeelezwa kwa ufasaha na mwandishi ambaye ingawa lugha yake ya asili ni Kiswahili ameweza kufinyanga lugha hiyo ya kigeni (Kiingereza) ili imtumikie yeye na amefaulu katika hilo. Baadhi ya wachapishaji wa vitabu vyake walitaka wayaondoe baadhi ya maneno na misamiati,

Endelea uk. 3

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com



Maisha ya Mtume Muhammad *saw*

Kutoka uk. 1

wake. Kwa hiyo wakaketi naye na kuanza kuyasikiliza maneno yake.

Akawaambia: "Ufalme wa Mwenyezi Mungu unakaribia kuja. Sasa masanamu yatafutwa duniani. Tauhidi (Umoja wa Mwenyezi Mungu) itastawishwa duniani. Wema na ucha Mungu utastawi tena duniani. Je watu wa Madina wako tayari kuikubali neema hii yenye shani kuu?"

Waliyasikiliza maneno yake na kuvutiwa nayo na wakasema: "Sisi twayakubali mafundisho yako. Kuhusiana na Madina kuipa hifadhi Islam au la, hilo itabidi turudi kwa watu wetu na kuongea nao na kisha mwaka ujao tutakuja tena kukuambia uamuzi wa watu wetu."

Watu hawa walirejea kwao na kuanza kuwapa ndugu na marafiki zao mafundisho yake (s.a.w.). Wakati huo huko Madina kulikuwepo na makabila mawili ya waarabu yanayoishi huko, makabila ya Aus na Khazraj pamwe na makabila matatu ya wayahudi ya Banu Quraidhwa, Banu Nadhwiir na Banu Qainuqa.

Watu wa makabila ya waarabu wa Aus na Khazraj walikuwa katika hali ya vita. Makabila ya kiyahudi ya Banu Quraidhwa na Banu Nadhwiir yalikuwa yameambatana na kabila la Aus na kabila la wayahudi la Banu Qainuqa likishirikiana na kabila la waarabu la Khazraj. Baada ya mapigano ya muda mrefu ikaanza kuwaingia hisia kwamba wanapaswa kufanya suluhu. Hatimaye baada ya kushauriana ikaamuliwa kwamba Abdullah bin Ubay bin Salul, aliyekuwa kiongozi wa kabila la Khazraj, ndiye awe mfalme wao wote.

Kutokana na mahusianao yao na Wayahudi, watu wa makabila ya Aus na Khazraj walikuwa wakizisikia mara kwa mara bishara zilizomo ndani ya Biblia. Wakati Wayahudi walipokuwa wakieleza hali ya misiba na shida zao, basi mwishoni walikuwa wakisema pia wakisema hivi kwamba: 'Nabii fulani anayefanana na Musa karibuni atadhihiri, wakati wake unakaribia. Atakapokuja sisi tutashinda tena duniani. Maadui wa wayahudi wataangamizwa. Hivyo watu wa Madina walipoyasikia madai ya Muhammad s.a.w. kutoka kwa wale mahujaji, ukweli wake (s.a.w.) ukatuama mioyoni mwao na wakasema kwamba yaonekana kama huyu ndiye yule yule Nabii ambaye Mayahudi walikuwa wakitupasha habari zake.

Hivyo vijana wengi sana wakaathirika na ukweli wa mtume wa Allah, Muhammad s.a.w. na bishara walizosikia kwa wayahudi zikawasaidia kuwaleta ndani ya imani.

Hivyo mwaka uliofuatia watu wa Madina wakaja tena Makka wakati wa Hijja. Safari hii watu kumi na wawili waliondoka Madina kwa dhamira hii kwamba wataenda kuingia ndani ya dini ya Muhammad s.a.w. Kati yao kumi walikuwa wa kabila la Khazraj na kumi wa kabila la Aus.

Wakakutana na Mtume Muhammad s.a.w. huko Mina na kufanya Baiat kwa kuushika mkono wake kwa kulikiri jambo hili kuwa hawatamuabudu yeyote minghairi ya Mwenyezi Mungu, hawataiba, hawatatenda maovu, hawatawaua mabinti zao, hawatasingiziana, wala hawatayaasi mafundisho mengine mema ya Nabii wa Mwenyezi Mungu.

Watu hawa waliporudi makwao wakaanza kuwahubiria watu wao kwa nguvu zaidi. Masanamu yakaanza kutolewa majumbani na kutupwa nje. Watu waliokuwa wakiinamisha vichwa vyao mbele ya masanamu wakaanza kutembea wakinyoosha shingo zao. Watu sasa wakawa hawako tayri kuinama mbele ya yeyote minghairi ya Mwenyezi Mungu. Wayahudi wakastaajabu kwamba kwa karne na karne za kuwa kwao marafiki wao wakiwahubiria, hawakuweza kuyaleta mabadiliko yaliyoletwa na Islam kwa watu hao kwa siku chache tu. Mawaidha ya Tauhidi (umoja wa Mwenyezi Mungu) yakawa yametuama barabbara mioyoni mwa watu wa Madina. Watu wakawa wanafululiza kuwajia Waislamu wakiwaambia: "Tufundisheni dini yenu!"

Lakini Waislamu hao wapya wa Madina sio tu kwamba hata wenyewe walikuwa hawana elimu kamili ya Islam, bali hata idadi yao haikuwa kubwa ya kuweza kuwaeleza kwa kina mamia kwa maelfu ya watu kuhusiana na Islam. Kwa hiyo wakamtuma mtu mmoja aende Makka kuomba wapatiwe sheikh. Na mtume s.a.w. akamtuma Madina kwa ajili ya kuihubiri Islam, sahaba mmoja aliyeitwa Mus'ab r.a. aliyekuwa amerejea kutoka Uhabeshi alikokuwa amekimbilia. Mus'ab r.a. alikuwa ni muhubiri wa kwanza wa Islam kutumwa nje ya Makka.

ISRAA

Ndani ya siku hizo hizo Mwenyezi Mungu Akampa tena bishara nyingine muhimu ihusikanayo na siku zijazo. Aliambiwa kwa kuonyeshwa katika Ruya fulani ya Kashfi kwamba ameenda Jerusalam na manabii wakasali sala nyuma yake. Jerusalem ilikuwa ni utabiri wa Madina iliyokuwa ije kuwa katika siku zijazo Markaz (Makao Makuu) ya ibada ya Mungu Mmoja. Na taabiri ya manabii kusali nyuma yake ilikuwa ni hii kwamba watu wa dini tofauti watajiunga na dini yake nayo itakuwa ni ya kimataifa.

Wakati huu hali ilikuwa mbaya sana kwa Waislamu huko Makka na shida zikawa zimefikia kiwango cha juu kabisa. Alipotoa taarifa ya kashfi hiyo watu wa Makka wakawa wamepata sababu nyingine mpya ya kukejeli na kudhihaki nao wakaanza kuifanyia dhihaka na kejeli ruya hiyo katika kila mikusanyiko yao. Lakini ni nani aliyekuwa akifahamu kuwa ujenzi wa Jerusalem mpya ulikuwa umeshaanza? Kaumu za watu wa Mashariki na Magharibi walikuwa wamesimama na kusikiliza kwa makini sana na kuisikiliza sauti ya nabii wa mwisho (wa kuleta sheria) wa Mwenyezi Mungu.

BISHARA YA USHINDI WA WARUMI

Itaendelea toleo Lijalo

Ni heshima na fahari kwa Tanzania

Kutoka uk. 2

yeye alikataa na akasisitiza kwamba ninazungumzia kwetu nilipozaliwa. Katika moja ya mahojiano aliwahi kusema 'mimi ninatoka huko. Akilini mwangu ninaishi huko.'

Athari za ukoloni. Upweke wa kuwa mbali na nyumbani. Jitihada za kuelewa utamaduni wa watu wengine. Ni ujumbe unaotawala katika kazi zake zilizompatia tuzo hii kubwa ya fasihi duniani. Kazi hizo ni pamoja na hadithi dupi na riwaya zifuatazo Memory of Departure, Pilgrims Way, Dottie, Paradise, Admiring Silence, By the Sea, Desertion, The Last Gift, Gravel Heart, Afterlives.

Wakati tunasherehekea heshima hii iliyoletwa na Abdulrazak Gurnah tuna mambo mawili matatu ya kujifunza. Mosi, ni jambo la kusikitisha kama alivyosema Nabii Isa a.s. kuwa Nabii haheshimiki kwao. Watanzania wangapi wanamfahamu shujaa huyu wa kalamu? Kama nchi tulifanya nini habari za kupewa tuzo hiyo zilipotufikia? Ni jambo la kuumiza na kusononesha kwamba sisi tunaotaka kuitangaza Tanzania hatuna vitabu vyake katika somo la fasihi katika shule zetu. Kwa hakika inasikitisha zaidi kwamba waandishi wetu maarufu vitabu vyao si sehemu tena ya somo la fasihi mashuleni. Ni vijana wangapi wa leo wamesoma vitabu vya Shaaban Robert, Mohammed Said Abdallah, Sheikh Kaluta Amri Abedi, Mathias Mnyampala? Tunatangazaje utamaduni wetu bila kutoa kipaumbele kwa waandishi wetu? Tulitumai kuwa wanaotangaza utamaduni wetu ili kuwavutia watalii waje kututembelea wangelikwenda Tanga kuzungumza na wale wanaomkumbuka au kumuona Shaaban Robert. Wangelifika pia katika kaburi lake na mashairi yake yangaliimbwa. Haya yote hayakufanyika. Na hatujachelewa

Endelea uk. 11

Askari wawili waikomboa Daluni



Na Rajabu Mkieti
Masjid Ihsan, Tanga

Katika ya Miaka 1990 joto la mahubiri ya jumuiya ya Ahmadiyya lilikua limepanda mkoani Tanga pamoja na nchi nzima ya Tanzania. Agizo la kiongozi wa jumuiya ya Ahmadiyya Duniani wa wakati huo. Khalifa Mtukufu IV Mirza Tahir Ahmad r.h lilikuwa ni kuhakiki tuongeza idadi ya waahmadiyya kwa kupata baiti nyingi. Jambo hilo ndilo lilikua lengo kuu.

Maulana Shekhe Bakri Abedi Kaluta wakati huo alikua akiongoza mkoa wa Tanga. Akiwa shekhe wa Mkoa hakufanya ajizi, alifanya hima akishirikia na wa Ahmadiyya wa Tanga mjini wakiwemo mzee Hatibu Tajiri, Bakari Tupa, Bakari Ruwa, Abdallah salimu Sefu wa Oman, Hashim chuma, Shafii kihaule pamoja na mzee Abasi Mkieti na wengine wengi wakiwa na hamu ya kutimiza agizo la khalifa wa zama kufanya mahubiri mengi na makubwa zaidi ambayo wataleta matunda na kupata waahmadiyya. Walifanya kazi hiyo na ikazaa matunda. Tanga ikawaka moto hakuna ulamaa yoyote aliyepima kina cha maji juu ya ukweli wa Hadharat Mirza Ghulamu Ahmadi a.s kila kona habari ya mjini ni Ahmadiyya. Mwenyezi Mungu akajalia kupatika kwa matawi katika sehemu kadhaa ikiwamo Mtiti, Shaurimoyo, Ugweno (Michungwani) pamoja na Daluni wakati huo ikiwa ni wilaya ya Muheza hivi sasa ni wilaya ya Mkinga mkoa wa Tanga. Jamaat ya Daluni ikiwa bado ni changa Mwalimu wa jamaati Ahmadiyya akapelekwa kwa kazi ya Malezi na kuongeza kasi zaidi ya mahubiri. Mwalimu wa jamaat akiwa tawini alifanya kazi yake punde muda haukupita Makao makuu ya jumuiya Ahmadiyya Tanzania ikatoa maagizo ya kumbadili shekhe Bakri kaluta kwenda mkoa wa Arusha na Shekhe Mubarak Ahmadi kuja Tanga.

Alhamdulilah shekh Mubarak Ahmadi alikua mgeni alipofika akiwa bado haja jipanga sawa sawa mtihani ukafika mtihani uliokuwa ni mkubwa sana ni nusura ya Allah ndio iliyoleta suluhu. Mwalimu wa tawi la Daluni akapata likizo tawi likabaki halina msimamizi. Mara Mashekh wa kisuni wakaiteka ngome yote ya Ahmadiyya katika tawi la Daluni. Uadui walio naomuda mrefu ukawa umepata upenyo wa kuudhihirisha. Tukio zima la utekaji lililofanyika lilikua na sura ya kupoteza hata usalama wa amani ya mji.

Waliweka msimamo Mashekh wote wa Maramba na Daluni kuwa hakuna mtu yoyote anayetakiwa kuusogelea msikiti wa Ahmadiyya pale kijiji, kama mtu atajaribu atarogwa au kupigwa mpaka Kufa kwa sababu Ahmadiyya ni makafiri na imani hii haitakiwi kabisa kuwepo katika mji huu. Waahamadiyya wote wa mji ule wakiwa bado ni wachanga wakaiacha imani yao huku wengine nyoyo zao zikiwa bado zipo katika Ahmadiyya lakini vitisho walivyo pewa viliwaadhiri na kuogopa kupoteza maisha yao. Taarifa ya kutekwa kwa waahamadiyya wa Daluni ikafika Tanga katika makao ya mkoa ya Ahamadiyya chumbageni masjid ihsani. Mtihani huu ulitokea kipindi cha Maulana shekhe Mubaraka Ahmad ulikua mkubwa mno kwani makao makuu ya jumuiya Ahmadiyya Tanzania wakiamini lipo tawi kumbe tawi limeshatekwa na Masheikh wa kisuni. Majlis Amila ya tawi la Tanga mjini ndio ilikua ikiongoza mapambano hayo ikakaa kikao cha haraka cha dharura kilicho ongozwa na Almaruhumu mzee Abasi Mkieti akiwa ndio Raisi wa wakati huo wa Tanga mjini.

Kikao kulikua ni cha moto kwani walitakiwa kutumwa watu, ila tatizo ni hali ya kupoteza usalama ndio ilikua shaka yao kubwa, kwani siku zote sifa ya Ahmadiyya ni kulinda amani na Masheikh wa kisuni wameahidi atakaye sogelea mji wao amani itapotea na kuwasaga tikitiki

Mwisho kikao kulitoka na maazimio kuwa kitafutwe kibali cha muhadhara ambayo ni haki ya kila kundi la kidini pili watumwe watu wasiozidi wawili ili wahakikishe wanajamati wanapatikana na kurudi katika Jama'at Ahmadiyya. Watu wawili ambao walitakiwa kutumwa ilikua ni njia za kiusalama na uchunguzi kama wakishindwa kuwarudisha waahmadiyya katika mji wa daluni watarudi na kuleta taarifa ili njia nyingine itumike. Shekh Mubaraka Ahmad hakutakikwa kwenda kwa sababu ya kiusalama pia ni mgeni na mazingira yake hayajui vizuri.Kura ya asikari wawili wa masihi Aliyeahidiwa ikawadondokea Abasi mngodo Mkieti na Bakari Juma Tupa. Hao ndio waliovishwa jukumu la kwenda kuikomboa tena Daluni na kulirudisha tawi hilo katika himaya ya Ahmadiyya. Malengo yalikua waenda wakae siku zisizo zidi tano yaliwekwa juu yao wahakikishe wanaikomboa tena Daluni. Wakapewa siku za kujiandaa. Siku ya jumamosi asubuhi safari ikaanza kuelekea kaskazini magharibi ya mkoa wa Tanga yaani Daluni walifika wakiwa na mabegi yao na vifaa vya sauti wakaviweka msikitini wakasali sala ya Adhuhuri na Alasiri kwa kuchanganya kisha wa kaenda katika Uwanja uliokusudiwa kufanyikia muhadhara. Walipofika kabla ya kuanza muhadhara mzee Abasi Mkieti alikwenda kwa Mwenyekiti wa kijiji kujitambulisha lakini alipofika ofisi ya mwenyekiti hali ilikua mbaya alifukuzwa na akarudi kwa swahibu wake kwenda kushauriana wakaona ni vyema kwenda kwa Mtendaji wa kata. Mzee Abasi mkieti alipofika ofisini akajitambulisha hali ikawa kama ya nyuma lakini hapa ilikua na afadhali basi katika maongezi kidogo akagundua kuwa yule Mtendaji wa kata ni kabila yake ni mbondei na yeye mzee Abasi ni mbondei hapo ikamlazimu mzee mkieti kubadili lugha akanza kumuhibiri yule Mtendaji kwa kibonde mara Mtendaji akaelewa waahamadiyya ni akinanani chuki ikaanza kuondoka akamuahidi kumpa ushirikiano na ulinzi kwa siku zote tatu za muhadhara.

MUHADHARA UNAANZA

Muhadhara ulianza huku uwanja ukiwa unawatu watatu mzee Abasi Mkieti, Bakari Tupa na Mtendaji wa kata. Mji ukiwa unazizima ukiwa na utulivu mkubwa spika sikitia sauti na kurusha mawimbi yake mbali hadi katika majumba ya wanakijiji na miji ya jirani ya daluni. Kweli kazi ya Mwenyezi Mungu daima ni kutegemea msaada wake. Kwani hakubahatika hata kwa akali kupita au kusogelea maeneo mtu hata mmoja kwa siku ile ya kwanza ya mkutano wa hadhara. Sawa na maelekezo ya kibali ilipofika saa 12 jioni wakafunga muhadhara walirudi msikitini na kujiandaa kwa sala na chakula. Wapata muda wa kupumzika kiasa baadae wakalala kwa zamu ili kufanya ulinzi isije akatokea wa kuwadhuru usiku ilipofika usiku wa saa nane wote wakaungana katika sala ya tahajudi hapo ndipo ilipofanyika dua maalumu ya kumuomba Mwenyezi Mungu ajalie ushindi katika kazi yao. Maombi hayo yalikua na umuhimu mkubwa kwani siku ya kwanza ilimalizika kukiwa hakuna dalili hata ya mafanikio katika kazi waliotumwa. Asubuhi ya siku ya pili ilipofika walijiandaa kwa kupita baadhi ya maandika kazaa ikiwamo kurani tukufu muda wa muhadhara ulipofika walifunga tena vifaa vya sauti kisa kazi ikaanza ratiba ya siku ya pili alianza kwa usomaji wa kuani tukufu mzee Abasi mkieti,ikafatiwa na mada ya pili juu ukweli wa Ahmadiiya mada hii iliwasilishwa na Mzee Bakari Juma Tupa wakati mada hii ikiendelea watu waakaanza kusogea katika kiwanja kile lakini ni wachache mada hii ilikua ni muhimu sana kwa wakati ule kwani moja ya hoja ya mashekhe wa kisuni waliyoisambaza kama silaha ya uadui wao nikuwa waahmadiyya sio waislamu. Maelezo yaliotolewa na mzee bakari tupa yalifuta uongo wote uliosambazwa na mashekhe wa kisuni kwani aliitumia kurani tukufu kudhihirisha ukweli wa ahmadiyya na kuendelea kwa utume baada ya mtukufu Mtume muhammadi saw.Mada yapili ndio iliondoa mzizi wa fitina kwani ilielezea ukweli juu ya uchawi na kurogwa mada hii ulikua na umuhimu wake kwani ahadi ya vitisho walivyopewa wale waahmadiyya wa pale kijijini ni kuwa kama wataendelea na kuwa waahmadiyya watarogwa. Mada hii iliwasilishwa na mzee Abasi mkieti. Mzee Abasi mkieti alitoa maelezo yaliofafanua juu ya ukweli kuhuu uchawi na alifanya rejea mbalimbali kudhibitisha uongo wa uchawi mwisho wa hutuba yake kasema "nawaambieni kweli kabisa yule ambaye ameewaahidi kuwaroga waahmadiyya ajiulize babu yake aliyempa hiyo tunguri yuko wapi? Hakika kama ameshafariki huyo babu yake nayeye hivi karibuni ataondoka na kuiacha hiyo tunguri na kumfata babu yake kama anao uwezo basi azuie kifo chake. lakini kama mna yakini juu ya alieumba mbinguni na dunia nawambieni hakuna mganga yoyote atakaye

Inaendelea uk. 5

Askari Wawili waikomboa Daluni

Kutoka uk. 4

wadhuru" wakati mada ya mzee mkieti ikifikia ukingoni tayari uwanja umesha jaa watu wakiwa na hamu ya kutaka kujua zaidi kwakuuliza maswali. Yule mganga ambaye alitaarishwa kuwaroga waahmadiyya alikua nyumbani kwake na sauti ya spika ilikua ikifika katika nyumba yake baada ya muda mfupi kupita mganga yule akipatwa na ugonjwa wa kiharusi na hakubahatika tena kuwaroga waahmadiyya bali yeye alishindwa kijitibu bali kwa kupitia ugonjwa huo akaambilia mauti. Baada ya muhadara hapo uwanjani palishwafika waahmadiyya kadhaa wakiwa na shauku na ari kubwa tena isio kifani kwani mzizi wa fitina umeshafika mwisho na Allah amewanusuru. Wakashirikiana na ndugu zao kuondoa vifaa na kurudi msikitini hakika ni Allah ndio anawaongoza watu walipo fika msikitini ilikua ni wakati wa sala ya magharibi hapo nmsikitini wakakuta zaidi ya asilimia tisini ya waahmadyya wameshafika kuwasubiri ndugu zao wa imani. Walisali sala ya magharibi na insha kwa kuchanganya baada ya hapo darasa kubwa la malezi juu kuwaimarisa ndugu hawa likafanyika. Allhamdulilah tawi la daluni liliweza kunusurika kupotea chini ya asikari wawili wa masihi Aliyeahidiwa,kama wasemavyo waswahili mti hujulikana kwa matunda yake tawi hili la daluni baada ya miaka kadhaa kupita tukio hilo ndilo lililotoa mwanachuoni mkuwa wa kiisilamu aliyetahasusi katika chuo cha Jamia Munashirini katika nchi ya Ghana afrika ya magharibu maulana shekhe Shabani Athumani shunda ambaye anahudumu hivi sasa katika studio ya Idhaa ya MTA Tanzania morogoro.Asikari hawa wawili wote wamesha fariki dunia mzee Abasi mkieti alifariki 1/06/2019. Mzee Bakari Juma tupa amezaliwa wilaya ya muheza kijiji cha Mindu amefariki dunia mwaka huu 13/07/2021 Innalillahi waina ilahi rajiuni hakiki sisi ni wa Allah na kwake tutarejea.mzee bakari tupa alikua muhubiri wa muda mrefu wa jumia ya ahmadiyya alijiunga na jumuia kupitia kwa mzee abasi mkieti kwani kwa asili ni ndugu yake upande wa mamazo.Mzee bakario Tupa yeye ni mmoja wa wwanzilishi wa tawi la mtiti na shaurimoyo mkoani Tanga Mwenyezi Mungu apokee juhidi yake hii katika dini amin.

Ni Wajibu kwa wanafunzi wa Kiahmadiyya Kufanya Mahubiri

Na **Zuhura Khalid Rufili**
Kivule DSM

Kwa kawaida ya waaminio ni kukumbushana katika kheri na kukatazana katika maovu baadhi ya wanafunzi wa kiahmadiyya tunajisahau katika suala zima la kufanya mahubiri. Kwa kiasi kikubwa tumekua tukiathiriwa na mafundisho ya kisuni kutokana na kutokujieleza kwetu kuwa ni waahmadiyya. Wewe kama mwanachuo au mwanafunzi wa sekondari una wajibu wa kumsaidia seyyidina Ahmad[as], katika kuieneza Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiya. sisi ndio wasaidizi wa seyyidina Ahmad[as] katika kufikisha ujumbe kutoka kwa Allah[sw] wengi wetu huko shuleni hatutambuliki kama Waahmadiyya bali tunatambulika kama Waislamu wa kawaida, kwa kuwa hatuoneshi utofauti kati yetu na wao. Jambo hili linapelekea kutokujulikana kwa Jamaat na kuonekana kuwa ni mpya miongoni mwa watu. Ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa[as] umetabiriwa kufika kila pembe ya dunia hivyo basi kama mwanafunzi wa kiahmadiyya uwe na shauku ya kufanikisha utabiri huu mpaka kutimia kwake. Uhubiri wa mwanafunzi unaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuieneza jamaat, kwa sababu wanafunzi wanaishi katika mkusanyiko wa watu wengi ambapo ni rahisi kufikisha ujumbe kwenye idadi kubwa ya watu tofauti na uhubiri wa MTU mmoja mmoja. Mwanafunzi wa kiahmadiyya usikubali kuwa na rafiki ama sehemu unayo ishi iwe shule ama nyumbani wasitambue kuwa wewe ni Ahmadiyya. Fanya mahubiri usijali kudharaulika Allah Atakulipa.

Tunayo mifano tofauti tofaut ya wanajamaat mashuhuri waliojaza baiat kwa kuhubiriwa na wanafunzi wa kiahmadiyya. Nao wanafunzi hao wamekuwa na mchango mkubwa katika kuieneza Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya. Hivyo tunatakiwa tuige mfano wa wanafunzi hao ili tuendeleze mbele jumuiya, kama tunavyoapa katika viapo vyetu vya tanzimu. Nitie mfano mmoja, kuna mwanafunzi wa kiahmadiya katika shule fulani, alimuona mwanafunzi wa kisuni ameshika kitabu cha Sala ya Kiislam cha Ahmadiya. Mwanafunzi wa kiahmadiyya akamuuliza mwanafunzi huyo kwamba anaelewa chochote kuhusiana na Jamaat Ahmadiyya? Mwanafunzi huyo akasema hapa yeye alipewa kama zawadi na rafiki yake ajifunze kusali, kwa hiyo hata hakuwa anajua kuwa rafiki yake ni Ahmadiyya. Kwa hiyo ni vizuri kumzawadia rafiki kitabu ila ujaribu kumpa mwangaza kidogo kuhusiana na jamaat, ili hata akisikia mahala pengine aweze kuelewa zaidi. Allah Atuwezeshe kushika uchamungu ili iwe rahisi kufanya mahubiri na pia Atufungulie mioyo yetu tuweze kukumbuka tunayokumbushwa, Amin.

Kifo Juu ya msalaba? Hoja kumi kutoka kwenye Biblia Takatifu

Kutoka toleo lililopita

1. ISHARA YA YONA.

Sasa tunaendelea na hoja zetu kutoka kwenye Biblia za kuonesha kuwa Yesu hakufia msalabani. Tunasoma katika Agano Jipya. ***Na makutano walipokuwa akimkusanyikia, alianza kusema, kizazi hiki ni kizazi kibaya, kinatafuta ishara, wala hakitapewa ishara kwa waniwawi, ndivyo atakavyokuwa mwana wa Adamu kwa kizazi hiki.*** (Luka 11:29-30).

Tena akasema, ***Akajibu, akawaambia kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa ishara, ila ishara ya Nabii Yona. Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu, mchana na usiku katika tumbo la nyangumi hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.*** (Yonah 1,17, 2:1,2).

Hapo Yesu Kristo analinganisha kadhia yake na ile ya Nabii Yona. Je Yona aliwapa ishara gani watu wa Ninawi. Biblia inasema: (Yonah 1,17, 2:1,2).

Bwana akaweka tayari samaki mkubwa ili ammeze Yona, naye Yona akawa ndani ya tumbo la samaki yule muda wa siku tatu, mchana na usiku. Ndipo Yona akamwomba Bwana, Mungu wake, katika tumbo la yule samaki akasema: Namlilia Bwana kwa sababu ya shida yangu naye akaniitikia, katika tumbo la kuzimu naliomba, nawe ukasikia sauti yangu.

Sawa na aya hizi za Biblia, Yona alimezwa na samaki mkubwa na kawa katika tumbo la samaki huyu siku tatu na mausiku matatu na hatimaye akatoka katika tumbo hilo

la samaki ilhali ni mzima. Hiyo ni ishara waliyopewa watu wa Ninevatani, Yona aliomba akaokolewa wakati yumo katika tumbo la samaki. Mungu alisikia maombi yake na Yona akatoka katika tumbo hilo akiwa ni mzima. Yesu anasema kizazi hiki kiovu na cha zinaa hakitapewa ishara isipokuwa kama ile ya Yona. Kwa hiyo ni nini kilicholeta kufanana baina ya ishara ya Yona na Yesu. Hakuna isipokuwa ukweli ya kwamba kuingia katika tumbo la samamki na kuingia katika moyo wa ardhina kutoka humo wazima. Yona na Yesu walilia kutokana na hayo yaliyowasibu na wakamuomba Mola awaokoe. Maombi ya wote wawili yalipokelewa. Kama Yesu hakuingia katika moyo wa nchi akiwa ni mzima na kutoka humo akiwa ni mzima, kuko wapi basi kufanana baina ya ishara hizi mbili? Yesu aliahidi kuonesha ishara moja tu kwa kaumu ya wakati wake, lakini hata kama ishara hiyo itathibitishwa kuwa si kweli, je kuna jingine la kuthibitisha madai yake ya kuwa Mtume? Kurejea kwa Yesu kwa ishara ya Yona ina maana ya kuwa hatakufa mslabani. Kwa hiyo kuna kila sababu ya kuamini kuwa nadharia ya kuzirai haikujengwa kwenye nadharia tete.

Itaendelea toleo Lijalo

Bustani ya Washairi

KUBETI

1. Imeshakua fasheni, kufanya yaso na mana
Najiuliza kwa nini, wanapotoka Vijana
Hamsikii kwa nini?, kamari iwe hapana
Moyo wangu waumia, vijana waangamia.

2. Kamari iwe hapana, isichezwe majumbani
Kukopa hela hakuna, sifanye ufirauni
Si usiku si mchana, mnajazana kumbini
Moyo wangu waumia, vijana waangamia.

3. Mnajazana kumbini, mnashindwa kupishana
Kutafuta milioni, mwaka mzima hakuna
Hamuoni hata soni, fanyeni kazi vijana
Moyo wangu waumia, vijana waangamia.

4. Fanyeni kazi vijana, mikeka ya kazi gani?
Mara kepu mara chana, una mkosi jamani
Badilika embu ona, unasubiria nini?
Moyo wangu waumia, vijana waangamia.

5. Unasubiria nini, kufanya vyenye maana
Muda mali kama nini, nakukumbusha kijana
Usije kuwa mgeni, wenzako wameshaona
Moyo wangu waumia, vijana waangamia.

6. Wenzako wameshaona, kamari ni ushetani
Embu fikiri kwa kina, ni mbaya kama ugoni
Na vijiwe vya mchana, mara baka mara mani
Moyo wangu waumia, vijana waangamia.

7. Nimeshafika mwishoni, nimesema vyenye mana
Jikiteni masokoni, pambana bado kijana
Msigande vibandani, kumuua barcelona
Tuendako si kuzuri, mnapotea vijana.

Abdallah Kalindima
K-mtoto

RABI TAKABALI DUA

Kwanza natoa salamu, kwa rijali na nisai,
Kwa jina lake Qayumu, Mola Mwenye asmai,
Naghani hii nudhumu, huku nafanya duai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

Tunakuomba Karimu, Allah Usiyelaghai,
Utushushie naimu, na Baraka anuai,
Utuwezeshe nidhamu, kuishika kwa uhai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

Ilahi Mola Dawamu, Uliyeumba samai,
Tulio kundini humu, tuepushe majidai,
Isije kutuhukumu, baiati tulobai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

Ya Rahmani Rahimu, Huna baba na Huzai,
Utuzishie hamu, ibada tusikinai,
Tuwe bora kwa kaumu, na maasi tuyasai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

Ewe mwenye Kurehemu, Twaomba yako liqai,
Waja wako mahamumu, tunatafuta shifai,
Tukinge na wadhalimu,wanotufanyia mai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

Laaliyu Laadhimu, manani Uliye Hai,
Endeleza kwa kudumu, ujio wa khulafai,
Wanoutilia ngumu, Allah watie nazai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

Ni wewe ndiye Alimu, tuepushie jinai,
Na utujaze elimu, sote tuwe ulamai,
Utufanye maasumu, daraja uturufai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

Ndiwe Azizu Hakimu, Sifazo hazichakai,
Tupe mahaba adhimu, ili tuwe ruhamai,
Na mbele ya mahasimu, utufanye ashudai,
Rabi takabali dua, nakuomba Rahmani.

Na Tumwa wetu Hashimu, Aliyeleta dhuhai,
Mpe Sala na Salamu, kwa ulufu na miai,
Ili siku ya kiyamu, atutakie shufai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

Na Masihi Muadhamu, huyu wetu Mirzai,
Mjaalie kaumu, ya wafasi hukamai,
Waifanye Islamu, iwashinde sufahai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani

Hapa natua kalamu, nipelee japo chai,
Niliyoyatakalamu, ni maombi si madai,
Ninaamini Rahimu, ya vilio hakatai,
Rabi takabali dua, nakuomba Rahmani.

Abdallah Hamis Mbanga (**Kungwi**)
Mtwara

ISHI KWA UNYENYEKEVU

Jina lako litukufu, siioni mithilie.
Nikuanzie raufu, barakazo nitilie.
Napindama mdhaifu, wewe ni kususdie.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Takabuli tahadhari, kwa unyenyekevu ishi.
Usijitie fahari, kuendekeza ubishi.
Kujiona u hodari, mbora wa matamshi.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Ati mimi ndo shupavu, ngangari kama mlima.
Wengine wote wachovu, nini kwangu watasema.
Unakosa usikivu,busara zake mnyama.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Mfa maji baharini, mzamivu maridadi.
Agongae baharini, dereva mwenye weledi.
We ni nani jamani, kujikweza kweza hadi.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Mwishoe unairuka, mipaka yake karimu.
Unaanza ushirika, unaacha isilamu.
Waona melimika, kumbe hauna elimu.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Kwamba wewe ndo tajiri, hakuna mtu afike.
Unajawa ujahiri, tangu pesa uzishike.
Ingawa kuna fahari, ni vipi asisikike.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Hadi kwenye uchamungu, wajiona mtimivu.
Unawapiga majungu, wengine ni wapotevu.
Unajifanya mzungu, kiswahili si sikivu.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahjdhari.

Si uturi si udwanzi, bali ni tele jalala.
Mungwa muelezi, udumu kumcha mola.
Sio yule mpuuzi, udumisha takabula.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli thadhari.

Ninamuomba rabuka, atutoe takabuli.
Atupe roho hakika, zenye mawazo mazuli.
Na sio zo kurupuka, zopungukiwa akili.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahadhari.

Hapa ndipo mwisho wake, ashiri beti zatosha.
Nilowapa myashike, wengine kuelimisha.
Moyoni na yawafike, lo ghafuri kukumbusha.
Ishi kwa unyenyekevu, takabuli tahdhari.

Bilaly Kaluta

KIZAZI_TEULE

Ni kizazi teule, Kijukuu cha sahaba
Kilo vikwa usukule, Kwacha ya dini mahaba
Kilo sahau ya kale, Kumbu ni visa nasaba
Siye warithi wa Yule, Masihi muahidiwa

Neema nyingi hulevya, Hula nguvu ya maombi
Rohoni Uja huavya, Kumfanya mja zombi
Salani huanza chovya, ndipo hugeuka pimbi
Zisitulevye laghui, Na anasa za dunia

Shunda Mshudia wana
Daluni, Tanga

NDIYO MAPENZI YA MUNGU.

Hongera kwa Muhariri, Kunitengea nafasi
Nami nipate dhukuri, Nitaruku nafsi
Niimbe langu shairi, Kwa wino na karatasi
Gazeti kufika leo, Ndio Mapenzi ya Mungu

Mungu akitaka jambo, hulitengea nafasi
Kisha akalipa umbo, Akalivisha libasi
Na kulitia urembo, Unyayo hadi utosi
Limedumu hadi leo, Ndiyo Mapenzi ya Mungu

Tangu lianze safari, Ni mbali sana kitambo
Miongo sasa dahari, Bado limeshika fimbo
Kama wimbi la bahari, Meli huzipiga kumbo
Hebu leo litajeni, Ndiyo Mapenzi ya Mungu

Sikuwepo siku zile, kiroho hata kiumbo
Ni wengi walisomile, Hili gazeti la tambo
Ndipo nasema simile, Enyi wajuzi wa mambo
Someni mlirudile, Ndiyo Mapenzi ya Mungu.

Gazeti lenye haiba, Nguvuze bado zitele
Bado linabeba huba, yake tumwa mteule,
Hadi hapo msalaba, ung'oke utoke pale
Tuunganike kwa hili, Ndiyo Mapenzi ya Mungu

Gazeti la mahubiri, Tangu zama za kale
Gazeti la washairi, Hasa wale wateule
Akili Mali mahiri, Akina Mpukutile
Wengi walipita shule, Ndiyo Mapenzi ya Mungu

Na mimi nilikutile, Gazeti la siku tangu
Likanibeba kwa lele, kukarimu tungo zangu
Miaka sasa itele, ni nyeupe nywele zangu
Gazeti Mwalimu wangu, Ndiyo Mapenzi ya Mungu

Wakatabu kalamu, nafupisha tungo yangu
Ingawa bado na hamu, kubarizi na wenzangu
Lakini yanilazimu, niwapishe na kwa tungu
Kusoma gazeti hili, Ndiyo Mapenzi ya Mungu.

A.R Mikila (**SIASA**)
Morogoro

KULISHA

Halishwi yeye hulisha, Rabi mtoa riziki
Sifa hino inatisha, nani anaimiliki
Nani aweza kuvisha, lau kapenda kaniki
Udongo walima pamba, nani kautengeneza?

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani, Migombani, Dar es salaam

HASIRA

Bisimilahi karima, nipe fasaha kusema
Yako mengi yanichoma, moyoni yananguruma
Nikiacha bila sema, kadamnasi mrama
Hasira moto mkali, jepushe uwe salama

Hasira mkali mwako, usio tone huruma
Kwa chochote kilichoko, haachi kikisimama
Tatengeneza ripuko, ufe au ukilema
Hasira moto mkali, jepushe uwe salama

Rafiki tamuunguza, utabaki ukilia
Mpenzi tampoteza, jeraha takuachia
Furaha hutoiwaza, majuto tajijutia
Hasira moto mkali, jepushe uwe salama

Jiepushe na hasira, wone raha ya maisha
Tabasamu kwenye sura, uzuri ukionyesha
Suluhu zenye busara, si hasira kuendesha
Hasira moto mkali, jepushe uwe salama

Hasira jiepusheni, umesimama we kaa
Na shari ziondoweni, aongea we nyamaa
Ugomvi uzuwieni, kubali ukikosea
Hasira moto mkali, jepushe uwe salama

Masihi Omary Kisagwa

Nguo chafu

Wanandoa wapya walihamia katika ujirani mpya. Asubuhi iliyofuata wakiwa wanapata kifungua kinywa, mwanadada huyo akamwona jirani yake akianika nguo nje. "Ile nguo sio safi sana", alisema "Hajui jinsi ya kufua kwa usahihi. Labda anahitaji sabuni bora ya kufulia". Mumewe alitazama, lakini alikaa kimya. Kila wakati jirani yake akining'inizia nguo yake ili ikauke, mwanandoa huyo mchanga alitoa maoni yaleyale.



Karibu mwezi mmoja baadaye, mwanamke huyo alishangaa kuona nguo nzuri safi kwenye mstari na akamwambia mumewe: "Angalia, amejifunza jinsi ya kufua kwa usahihi. Ninashangaa ni nani aliyemfundisha hili."

Mume alisema, "Niliamka asubuhi na mapema na kusafisha madirisha yetu."

Funzo: Ikiwa madirisha yetu ni machafu ndivyo tutawaona wengine kuwa wachafu pia. Kile tunachokiona kwa wengine ni kielelezo cha utu wetu wa ndani! Ndivyo ilivyo kwa maisha kwamba kile tunachokiona tunapotazama wengine kinategemea usafi wa dirisha ambalo tunatazama. Ni rahisi kwetu kujadili watu wengine, maisha yao na mambo ambayo kwa kweli hayatuhusu na tunaelekea kusahau - madirisha yetu yanaweza yasiwe safi kiasi hicho! Tukiwa wema tutaona mema...

Katika maisha mara nyingi sisi huwa na tabia ya kuhukumu na mara nyingi sana huwadharau wengine bila kuchunguza kwa undani zaidi kwa nini mtu huyo ana tabia kama hiyo.

Imepokewa kuwa Mtume kipenzi cha Mwenyezi Mungu (Swalla Allaahu ‹alayhi wa aalihi wa sallam) amesema: "**Muislamu ni kioo kwa Muislamu mwingine.**" (Abu Dawud).

CHEMSHA BONGO

Kuna wanyama wangapi katika picha?



UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Jinsi ya kupika Keki ya maziwa

Na **Mtandao**



MAHITAJI

1. Siagi Kikombe 1
2. Sukari Kikombe 1
3. Unga Vikombe 2
4. Maziwa 1/2 (nusu) Kikombe
5. Mayai 4
6. Baking Powder 1 Kijiko cha supu

JINSI YA KUPIKA CAKE YAKO

1. Washa oveni 350 - 400 Deg C liache lishike moto huku ukitayarisha mchanganyiko wa keki.

2. Changanya sukari na siagi mpaka ichanganyike.

3. Mimina mayai na maziwa uchanganye vizuri.

4. Mimina Baking Powder kwenye unga na uchanganye vitu vyote pamoja.

5. Endelea kuchanganya vizuri mpaka uhakikishe vimechanganyika vizuri (unaweza kufanya bila ya mashine)

6. Chukua trey ambayo haitojaa ukiimimina, ipake siagi na umimine mchanganyiko wako. Treya isiwe nzito sana au nyepesi sana bali iwe wastani.

7. Ipike (Bake) mpaka iwive.

8. Epua iache ipoe ndio ukate kate vipande.

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA*as*

Amri za Huruma

Hazrat Masih Maud a.s anasema: Likumbukeni vyema jambo hili pia kwamba ziko Amri za Mwenyezi Mungu. 1. Ya kwanza ni hii kwamba usimshirikishe na yeyote, si katika dhati Yake, sifa Zake wala Ibada Zake. 2. Na ya pili, muwarehemu wanadamu wengine. Na mradi wa Hisani sio huu kwamba uwafanyie ndugu zako na Jamaa zako tu hisani, bali yeyote yule, Mwanadamu au Kiumbe yeyote miongoni mwa Viumbe wa Mwenyezi Mungu, bila kujali yu Baniani au Mkristo. Ninakuambieni kweli kuwa Mwenyezi Mungu Amechukua jukumu la kuwapatieni uadilifu; Hapendi mjifanyie wenyewe. Kadiri mtakavyokuwa na Upole, Huruma na Unyenyekevu, ndivyo Mwenyezi Mungu Atakavyofurahishwa nanyi. Wakabidhini maadui zenu kwa Mwenyezi Mungu. Kiama kipo karibu, hampaswi kufadhaishwa na matatizo hayo wanayokupeni maadui. Mimi naona kwamba bado mtapata usumbufu sana toka kwao, kwa sababu wale watu walio nje ya wigo wa ustaarabu ndimi zao hubwatuka kana kwamba bwawa limebomoka na kusababisha mafuriko, hivyo mfuata dini anapaswa kuudhibiti ulimi wake.

(Malfudhat, J. 9, uk. 164 - 165)

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

Matendo ya Fadhili na Rehema za Allah

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

(وَيُطْعِمُونَ الطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا * إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنْكُمْ جَزَاءً وَلَا شُكُورًا)

9. *Na huwalisha chakula maskini na yatima na mfungwa kwa mapenzi Yake. (Husema): Tunawalisheni kwa ajili ya radhi ya Mwenyezi Mungu tu, hatutaki kwenu malipo wala shukurani.* Surah 76:9-10

Masih Aliyeahidiwa a.s anasema: 1. Ombeni Dua, 2. Mtubu na 3. Muwe mkitoa Sadaka ili Mwenyezi Mungu Akutendeeni kwa Fadhili na Rehema zake (Malfudhaat, J.1, UK. 134 - 135 chapa mpya).

Kuhusu Kuomba Dua na Kutubu Masih Aliyeahidi a.s Anasema: Yapaswa kila Mtu ajitahidi kuamka kwa ajili ya Kusali Sala ya Tahajjud, na pia Muombe Ombi la QUNUT katika Sala tano. Mtubie kwa kila jambo lenye kumkasirisha Mungu. Mradi wa toba ni huu kwamba muayaache yale maovu yote na yale yasababishayo hasira as Mwenyezi Mungu na kufanya mabadiliko ya kweli na mpige hatua mbele na kushika Uchamungu, humo pia mna Rehema ya Mwenyezi Mungu.

Sadaka huleta Msamaha na Ukarimu/ Upole 2:268-269 kuhusu jambo hili Masih Aliyeahidiwa a.s Anasema: Enyi Marafiki! Ishikeni kwa nguvu desturi hii: Watendeeeni watu wa kila kaumu kwa UPOLE. AKILI Huongezeka kutokana na Upole, na FIKRA Zenye KINA Huzalika kutokana na Ustahimilivu... (Tablighe Risalat, J.6, uk. 170).

Eeh Allah, Wewe ndiwe Mlinzi wetu, basi tusamehe na Uturehemu, nawe ndiwe Mbora wa kughofiri. Amin

NUKUU YA HADITHI

Na **Ustadhi Issa Malenge** - 0625 914 740 0752 334 332

وعن أَبي العباس سهل بن سَعد الساعِدِيّ رضي الله عنه أنَّ رَسُول الله صلى الله عليه وسلم بَلَغَهُ أنَّ بَني عَمرو بن عَوْفٍ كَانَ بَيْنَهُمْ شَرٌّ، فَخَرَجَ رسولُ الله صلى الله عليه وسلم يُصْلِحُ بَينَهُمْ في أُنَاس مَعَهُ، فَحُبِسَ رَسُول الله صلى الله عليه وسلم وَحَانَتِ الصَّلاة، فَجَاءَ بِلالٌ إِلَى أَبِي بكر رضي الله عنهما، فَقَالَ: يَا أَبَا بَكْر، إِنَّ رَسُول الله صلى الله عليه وسلم قَدْ حُبِسَ وَحَانَتِ الصَّلاةُ فَهَلْ لَكَ أَنْ تَؤُمَّ النَّاس؟ قَالَ: نَعَمْ، إِنْ شِئْتَ، فَأَقَامَ بِلالٌ الصَّلاةَ، وتَقَدَّمَ أَبُو بَكْرٍ فَكَبَّرَ وَكَبَّرَ النَّاسُ، وَجَاءَ رَسُولُ الله صلى الله عليه وسلم يَمْشِي فِي الصُّفُوفِ حَتَّى قَامَ فِي الصَّفِّ، فَأَخَذَ النَّاسُ فِي التَّصْفِيقِ، وَكَانَ أَبُو بكرٍ رضي الله عنه لا يَلْتَفِتُ فِي صَّلاتِه، فَلَمَّا أَكْثَرَ النَّاسُ فِي التَّصْفِيقِ الْتَفَتَ، فإِذَا رَسُول الله صلى الله عليه وسلم، فَأَشَارَ إِلَيْه رسولُ الله صلى الله عليه وسلم فَرَفَعَ أَبُو بَكْر رضي الله عنه يَدَهُ فَحَمِدَ اللهَ، وَرَجَعَ القَهْقَرَى وَرَاءهُ حَتَّى قَامَ فِي الصَّفِّ، فَتَقَدَّمَ رَسُولُ الله صلى الله عليه وسلم، فَصَلَّى للنَّاسِ، فَلَمَّا فَرَغَ أَقْبَلَ عَلَى النَّاسِ، فَقَالَ: ((أَيُّهَا النَّاسُ، مَا لَكُمْ حِينَ نَابَكُمْ شَيْءٌ فِي الصَّلاةِ أَخَذْتُمْ فِي التَّصفيق؟! إِنَّمَا التَّصفيق للنِّساء. مَنْ نَابَهُ شَيْءٌ فِي صَلاتِهِ فَلْيَقُلْ: سُبْحَانَ الله، فَإِنَّهُ لا يَسْمَعُهُ أحدٌ حِينَ يقُولُ: سُبْحَانَ الله، إلا الْتَفَتَ. يَا أَبَا بَكْر: مَا مَنَعَكَ أَنْ تُصَلِّي بالنَّاسِ حِينَ أَشَرْتُ إِلَيْكَ؟))، فَقَالَ أَبُو بَكْرٍ: مَا كَانَ يَنْبَغِي لابْنِ أَبِي قُحَافَةَ أَنْ يُصَلِّي بالنَّاسِ بَيْنَ يَدَيْ رَسُول الله صلى الله عليه وسلم. مُتَّفَقٌ عَلَيهِ.

Abdul Abbas Sahl bin Sa'ad*ra* anasimulia kwamba Mtume*saw* alipata khabari ya ugomvi uliotokea kati ya watu wa Bani Amr bin Auf. Mtume*saw* akatoka na kwenda pamoja na baadhi ya Maswahaba kuwapatanisha. Huko alizuwiwa kwa ajili ya kukutana na watu hata wakati wa sala ukafika.

Bilal alimwendea Abu Bakar*ra* na kumwambia kuwa Mtume*saw* amezuwiliwa huko na sasa ni wakati wa sala utaweza kusalisha watu? Yeye akaitikia na kusema ndiyo, kama ukitaka. Bilal akasoma Iqama na Abu Bakar*ra* akaenda mbele na sala ikaanzishwa.

Mara Mtume*saw* akafika na kwenda moja kwa moja akipita kati kati ya mistari na kusimama katika safu ya kwanza. Hapo waliokuwa wanasali wakaanza kupiga makofi. Abu Bakar*ra* akaendelea kusalisha na hakujali. Makofi yalizidi naye akamuona Mtume*saw* yuko huko na kwa ishara akamuongoza Abu Bakar*ra* aendelee kusalisha. Lakini Abu Bakar*ra* akainua mikono yake na kusema Alhamdulillah akarudi nyuma na kuingia katika safu. Mtume*saw* akasogea mbele na kusalisha.

Sala ilipokwisha alikaa akiwageukia waliokuwa nyuma yake na kuwaambia. Kwa nini nyinyi mnapiga makofi mkiwa ndani ya sala? Linapotokea jambo fulani kupiga makofi ni kazi ya wanawake tu. Lakini mnapoona jambo lolote limetokea mkiwa ndani ya sala semeni **Subhanallah** (Mwenyezi Mungu ni mtukufu). Hiyo itatosheleza moyo. Na wewe Abu Bakar kwa nini hukuendelea kusalisha hali mimi nilikutolea ishara uendelee?

Yeye akajibu: Haifai kwa mwana wa Abu Kahafah kuongoza sala mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. (Bukhar na Muslim).

MATUKIO KATIKA PICHA



Mashindano ya hotuba ya Kiarabu Jamia Ahmadiyya Morogoro, Tanzania



Kambi ya Malezi iliyofanywa kwa wiki 3 Shinyanga





Kambi ya Malezi Mkoani Shinyanga iliyofanyika tangu 24 Agosti hadi 18 Septemba 2021



Wanafuzi wa Jamia Ahmadiyya Tanzania wakicheza mchezo maalum wa Baa'ri



Kambi Ya Malezi (Refresher Course) Geita





Kambi Ya Malezi (Refresher Course) Geita

Heshima na Thawabu kwa Waahmadiyya



Na **Sheikh Muzaffar Durrani**
Rabwah, Pakistan

Waahmadiyya wamepata heshima na thawabu nyingi kwa kumpokea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Seyidna Ahmad as aliyetumwa kama msadikishaji na msaidizi wa Mtume Muhammad saw. Seyidna Ahmad as akieleza heshima hizo ameandika katika kitabu chake kiitwacho Kuondoa wasiwasi.

Heshima tano:

Awali ni hii kuwa, wao wamejenga dhana njema kwa ndugu yao (Seyidna Ahmad as) na hawakumchukulia kuwa muongo, na hawakuruhusu kupenya moyoni aina yoyote ya shaka chafu dhidi yake. Kutokana na sababu hii wamestahiki kupata thawabu hii anayopata mtu katika hali ya kuweka dhana njema kwa ndugu yake.

Pili, ni hivi kuwa hao wakati wa kuikubali haki hawakuogopa kulaumiwa na yeyote mwenye fundo la lawama yake, wala hawakuzidiwa na jazba za nafsi. Ndiyo maana, kwa sababu hii wamestahiki thawabu, kuwa wao baada ya kuupokea wito wa haki na baada ya kusikia sauti ya mnadi mmoja wa kiungu wakaupokea ujumbe wala hawakusita kutokana na kikwazo chochote kile.

Ya tatu ni hii kuwa, kwa sababu ya kuamini msadikishaji wa bishara, wameondokana na wasiwasi wote unaozalika siku moja kutokana na kusubiri sana kwa muda mrefu. Na mwisho katika hali ya kukata tamaa husababisha kupotea imani. Na wale watu wema, sio tu kwamba wameepukana na hatari zilizoelezwa hapo juu bali ishara moja ya Allah na bishara ya Nabii wake kwa kuziona kutimia katika uhai wao wamezidi sana katika nguvu ya imani na kupata maarifa ya imani iliyokuwa imani ya kusikia tu awali. Sasa wameepukana na wasiwasi zote ambazo huwa zinazozalika mioyoni juu ya bishara hizo ambazo huwa hazifikii kutimia.

Ya nne ni kuwa hao kwa kumwamini Mjumbe aliyetumwa na Mwenyezi Mungu wameepukana na zile kali na ghadhabu za Mungu ambazo huwa zinawapata waasi ambao huwa hawapati hisa yoyote isipokuwa kukadhibisha na kukataa.

Ya tano ni hii wamekuwa wamestahiki kupata zile neema na baraka zinazowateremkia wale watu waaminifu ambao kwa mawazo mema wanamkubali yule anaekuja kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Hizi ndizo zile faida ambazo Inshallah kwa fadhili za Mwenyezi Mungu watazipata wale watu waliomkubali Imamu wa zama.

Dhana mbaya ya wapinzani:

Lakini wale watu wasiokubali wao wanakosa mema yote haya na fikra, hofu na wasiwasi wao huu ni batili kuwa katika hali ya kukubali dini itapata madhara. Siwezi kuelewa kwamba kwa sababu gani hasara inaweza kutokea kwa dini. Hasara ingekuwa katika sura hii kuwa kama angekuwa analazimisha kufuata elimu mpya ya Kiislamu kinyume cha mafundisho ya dini ya Islam; kwa mfano angeharamisha kitu kilicho halali au angehalalisha kilicho haramu. Au angebadilisha itikadi za kiimani zilizolazima kwa ajili ya ukovu, au angeongeza au kupunguza kitu katika vitendo vya kisheria kama vile sala, saumu, hija na kutoa zaka n.k. Kwa mfano mahali pa kusali sala tano angefanya mara kumi au angeacha ikawa mara mbili tu au saumu za mwezi mmoja angefaradhisha ziwe za miezi miwili au angepunguza, au angeelekeza ziwe pungufu zaidi ya hapo; Hapo bila shaka upungufu ungekuwepo bali ni kufuru na hasara. Lakini katika hali ambayo anasema hivi hivi mara kwa mara kuwa "enyi ndugu, mimi sikuja na dini mpya wala mafundisho mapya bali mimi natoka miongoni mwenu na ni Mwislamu kama ninyi. Na kwa ajili yetu sisi Waislamu, isipokuwa Kurani Tukufu hakuna kitabu chochote kile tunachoweza kukifuata au kuwaongoza wengine kukifuata. Wala hakuna kiongozi wala mfuatwa wetu mwingine ila yule Muhuri wa Manabii, Muhammad saw."

Hatuna wasiwasi:

Sasa kwa ajili ya Mwislamu mstawi yeyote kuamini dai lake hili lenye msingi wa ufunuo Kutoka kwa Allah, kuna pahali pa wasiwasi gani. Kwa mfano tu kama kashfi na funuo zake ni makosa na maagizo anayopewa yeye amedanganyika kuyaelewa, sasa kwa anayekubali kuna kosa gani? Je atakuwa amekubali jambo ambalo litamsababishia ufa wowote katika dini yake? Kama kweli kweli katika uhai wetu Hadhrat Isa Ibnu Mariam huyo huyo akishuka kutoka mbinguni, basi moyo wetu utafurahi na macho yetu yatangaara. Sisi kwa Jumuiya yetu itakuwa wa kwanza kumpokea na itapata thawabu ya kukubali jambo la awali lilolikubali kwa nia safi na kwa kumhofu Mwenyezi Mungu; hata hivyo katika hali ya kosa hilo pia (kama ikidhaniwa kuwa) hatua yetu ya thawabu itaendelea kuwa mbele. Sisi tumepata thawabu mbili na wapinzani wetu moja tu. Lakini kama sisi ni wakweli na wapinzani wetu ni wenye makosa kwa kuweka matumaini ya siku za baadaye basi imani za wapinzani wetu zimo katika hatari kubwa sana. Maana kama wao katika uhai kweli kweli wamemuona Nabii Isa bin Mariam katika hali ya jalali na utukufu anashuka kutoka mbinguni na wamemshuhudia kwa macho yao akishuka akiambatana na malaika, hapo ndipo imani yao itakuwa imesalimika, waila katika hali ingine ya pili imani haionekani itabakia salama. Kwani kama mpaka kufikia mwisho wa uhai wao mtu yeyote hakuonekana akishuka kutoka mbinguni bali wenyewe walikaribia kufa. Hivyo ni dhahiri kuwa watakwenda nazo shaka kemkem na juu ya bishara za Nabii Mkwelisaw wasiwasi za aina aina za wazi wazi zitazalika moyoni. Na ni karibu kuwa wasiwasi mkali wa aina fulani utokee utakaosababisha hata imani pia iangamie. Kwani zama hizi kwa mujibu wa ishara za Injili na Hadithi ni zama hizi hizi ambamo Masihi Mauud anatakiwa ashuke. Ndiyo maana miongoni mwa watawa waliopita wenye kashfi, ndani ya kashfi zao wamebainisha kuwa muda wa kuja kwa Masihi ni miaka ya mwanzoni mwa karne ya kumi na nne ya Kiislamu.

Mshusheni Masihi:

Hivyo basi kama Seyidna Ahmad as sio Masihi mauud, basi ninyi watu mshusheni Masih Mauud kutoka mbinguni. Basi ninyi mu wazao wa watawa, kaeni msikitini muombe dua kwa unyenyekevu mkubwa kuwa Isa Ibnu Mariamu aje kutoka mbinguni huku ameweka mikono juu ya mabega ya malaika ndipo mtakuwa wakweli waila kwa nini basi ninyi mnafanya dhana mbaya pasipo na haki na mnakuwa mnakuja chini ya tuhuma ya aya hii: Usifuate usiyo na elimu nayo. (Banii Israaiil, 17:37) Muogopeni Mwenyezi Mungu.

Kwa fadhili ya Allah Jumuiya yetu ni Jumuiya jema ambalo kwa wakati wake limemkubali mamuri aliyetumwa na Mungu wa mbingu na ardhi. Na mioyo yao haikuona ajizi yoyote katika kukubali kwa sababu wao walikuwa wema na Mwenyezi Mungu amewachagua kwa ajili yake, Mungu Akawapa nguvu na wengine hawakupewa na akawafunulia vifua vyao na wengine hawakufunulia. Hivyo basi wale waliochukua, hawa wataongezewa zaidi, lakini wale ambao hawakuchukua vitachukuliwa kwao walivyokuwa navyo hapo kabla. Waongofu wengi walitamani kuwa wazione zama hizi, lakini hawakuweza kuziona. Lakini ni masikitiko kuwa watu hawa wameona lakini hawakukubali.

Mfano wa wapinzani:

Kuhusu wao mfano huu unatosha kuwa hivi kwamba mfalme mmoja kwa mujibu wa ahadi yake akamtuma mtawala mmoja kwenye mji fulani ili aone kwa hakika mtii ni nani? Na asietii ni nani? Na ili magomvi yote yaliyomo ndani yao yaamuliwe. Hivyo basi mtawala huyu akafika katika muda huo huo uliokuwa lazima kwake, naye akawafikishia ujumbe wa kiongozi wake na akawaita wote kwa njia iliyoongoka na akadhihirisha kuwepo kwake hakimu. Lakini hao wakapata mashaka juu ya kuwa kwake mtumishi wa serikali, ndipo akawaonyesha alama zinazohusiana na watumishi wa serikali tu. Lakini wao hawakuamini wala kumkumkubali nao wakamtazama kwa mtazamo wa karaha nao wakajiona wakubwa na wakakataa kumkubali kama hakimu. Bali wakamshika na kumfedhehesha na wakamtemea mate usoni, na wakakimbilia kumuua. Wakamwona mnyonge na duni na wakamwona hakiri na wakampinga kwa matusi makali. Kisha baada ya kuteswa sana kwa mikono yao iliyopangwa naye akarejea kwa mfalme wake. na wale watu wote waliomfanyia vibaya kiasi hicho wakaendelea kumsubiri mtawala mwingine aje na njia ya ujahili wakaendelea kudumu kwenye mawazo haya haya batili kuwa huyu hakuwa mtawala bali yule ni mtu mwingine atakaekuja ambaye sisi tunatakiwa kumsubiri. Hivyo basi wakamsubiri mtu huyo mchana kutwa nao walikuwa wanasimama na kumchungulia kuwa atakuja lini na waliendelea kuizungumzia ahadi ya mfalme, na waliendelea kumsubiri tu

Endelea uk 11

Makhalifa Walioongoka - Hadhrat Umar ibn Al-Khattab ra

Kutoka uk. 12

mkataba ulipokamilika Hadhrat Umar ra akaenda Baitul Maqdas. Hadhrat Umar ra alipofika alikuwa amevaa mavazi ya kawaida kabisa. Waislamu walikuwa na wasiwasi kuwa Wakristo watafikiria nini, ndiyo maana wakamwomba Hadhrat Umar ra avae mavazi ya fahari. Hadhrat Umar ra akajibu kuwa heshima ya Uislamu tuliyopewa sisi inatosha vizuri na haihitaji kuvaa mavazi yoyote ya fahari. Wakristo walipomwona Hadhrat Umar ra wakajazwa na hisia za heba na adhama ya kuwepo kwake. Hapo Wakristo wakamkabidhi Hadhrat Umar ra funguo za mji wa Baitul Maqdas. Hadhrat Umar ra akatembelea Baitul Maqdas na wakati wa Sala ulipowadia, Wakristo wakamkaribisha asali kanisani. Lakini Hadhrat Umar ra akakataa na kusema kuwa yeye anahofu kuwa akifanya hivyo, Waislamu wataichukulia sehemu hiyo kuwa mahali patakatifu na watajaribu kupokonya kanisa hilo. Kwa hivyo, Hadhrat Umar ra akaondoka na kusali nje ya kanisa. Khalifa Mtukufu atba alisema kuwa viongozi wa jeshi la Waislamu wakaanza kumkaribisha Hadhrat Umar ra katika karamu zao. Lakini Hadhrat Abu Ubaidah Bin Al Jarrah ra hakumkaribisha Hadhrat Umar ra na alipoulizwa sababu ya kutomwalika karamuni akajibu kuwa akimkaribisha Hadhrat Umar ra, yeye hataweza kuzuia machozi yake yasitiririke. Hata hivyo, wote hao wawili siku moja wakaelekea kwenye hema ya Hadhrat Abu Ubaidah ra na ndani ya hema yake mlikuwa hamna chochote isipokuwa matandiko ya farasi aliyoyatumia Hadhrat Abu Ubaidah ra kama malazi yake na vipande vya mkate uliokauka vilivyokaribishwa na kikombe cha maji na chumvi. Hadhrat Umar ra alipoyaona mandhari haya akapatwa na machozi na akamkumbatia Hadhrat Abu Ubaidah ra.

Hadhrat Syedna Bilal ra Alitoa Adhana Tena:

Khalifa Mtukufu atba alisema kuwa katika Eliya watu wakamwomba Hadhrat Umar ra amwamuru Hadhrat Bilal ra atoe adhana. Hadhrat Bilal ra alisema kuwa alikuwa ameahidi baada ya kifo cha Mtume Mtukufu Muhammad saw kwamba hatatoa adhana tena maishani mwake. Lakini kwa vile Ameerul Mumineen Hadhrat Umar ra amemwomba basi amekubali kutoa adhana. Adhana yake ikawakumbusha Masahaba ra wote zama za Mtume Mtukufu Muhammad saw na wote wakatokwa na machozi.

Uwezo wa Kimkakati wa Hadhrat Umar ra wa Kushinda Jaribio Kubwa:

Khalifa Mtukufu atba alisema kuwa Waislamu walipoendelea kuupata ushindi siku hadi siku, watu na wakazi wa miji wakawa na hofu ya kuupoteza utawala wa miji yao. Wakazi wa Jazirah eneo fulani lililopatikana baina ya Syria na Iraq wakamwandikia Hirakal barua ya kuomba msaada na wakamwomba atume meli za kijeshi za Warumi ili kupigana na Waislamu. Mfalme Hirakal akakubali kuwasaidia, kwa vile akadhani kuwa mpango wake utafaulu. Wakazi wa Jazirah walipojua kuwa Hirakal amekubali ombi lao, wao wakatuma jeshi la watu elfu thelathini kwenye eneo la Homs. Hadhrat Abu Ubaidah ra akapata habari za njama na hila hizo. Yeye akashauriana na Hadhrat Khalid Bin Walid ra, nao wakakubaliana kuwa kwa kupigana na maadui, yafaa wakusanye jeshi zima la Waislamu kusini mwa Syria. Meli za Hirakal zilipofika ufukoni, Waislamu wakajikuta katika hali ngumu. Hadhrat Abu Ubaidah ra akamwandikia Hadhrat Umar ra barua na kumwelezea hali hiyo ya kutisha. Hadhrat Umar Bin Al Khattab ra alimwamuru Hadhrat Sa'ad Bin Abi Waqaas ra atume usaidizi, naye akalituma Homs jeshi la watu 4,000. Hata hivyo, idadi hii haikutosha kwa kupigana na jeshi la wakazi wa Jazirah. Lakini jeshi la Jazirah lilipokuwa mjini Homs, Hadhrat Umar ra akaamrisha kuwa jeshi lingine litumwe Jazirah, ili jeshi la wakazi wa Jazirah lilazimike kurudi Jazirah kwa kutetea miji yao. Hiyo ikaonyesha uwezo wa kimkakati wa kipekee wa Hadhrat Umar ra, jeshi la Jazirah likalazimika kuacha Homs na kurudi Jazirah. Mwishowe, Waislamu wakawa washindi.

Khalifa Mtukufu atba alisema kuwa ataendelea kueleza matukio ya maisha ya Hadhrat Umar ra katika hotuba zijazo.

Sala ya Jeneza:

Khalifa Mtukufu atba alisema kuwa ataongoza Sala ya Jeneza ya Wanajumuiya hawa waliofariki dunia:

Chaudhari Said Ahmad Lakhan:

Bw. Chaudhari Said Ahmad Lakhan alikuwa anaishi Canada. Yeye alikuwa mjukuu wa Sahaba wa Hadhrat Masihi Mau'd as. Aliacha wana sita na mabinti watatu ambao wote wanaitumikia Jumuiya kwa njia moja au nyingine. Mwana wake mmoja aitwaye Sheikh Faheem Ahmad Lakhan ni Mbashiri katika Kenya na hakuweza kushiriki katika mazishi ya baba wake.

Khalifa Mtukufu atba aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Amjaalie subira. Bw. Chaudhari Said alikuwa na adhama ya hali ya juu sana kwa imani yake na kwa Hadhrat Masihi Mau'd as. Alikuwa akiwanasihi watoto wake kila wakati kwamba wasiwe na hofu ya mtu yeyote yule kuihusu Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Khalifa Mtukufu atba aliomba kuwa Mwenyezi Mungu Amtendee kwa ghofira na rehema. Ameen.

Muhammad Shahabud Din:

Bw. Muhammad Shahabud Din aliyekuwa anahudumu kama Naibu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Bangladesh. Huyo alikuwa na sifa nyingi njema na alikuwa na upendo wa hali ya juu kwa Ukhalifa. Ameacha wana wanne na mabinti watatu. Akakabiliwa na upinzani kwa jamii yake pia, lakini akauvumilia kwa subira sana. Alikuwa mtu mwaminifu sana. Khalifa Mtukufu atba aliomba kuwa Mwenyezi Mungu Amtendee kwa ghofira na rehema. Ameen.

Raul Abdullah:

Bw. Raul Abdullah mwanajumuiya wa Agentina. Huyo alikuwa katika wanajumuiya wa mwanzo wa Agentina. Akapata habari kuihusu Jumuiya mara ya kwanza katika monyesho ya vitabu, na ingawa watu walijaribu kumkengeusha kutoka Jumuiya, hata hivyo yeye alikuwa akishiriki katika mipango ya Jumuiya. Yeye akashiriki katika Jalsa Salana Uingereza kwa kuondoa shaka zote zilizokuwa akilini mwake. Na baada ya kukutana na Khalifa Mtukufu atba akawa na yakini na akajiunga na Jumuiya. Alikuwa na adhama kubwa moyoni mwake kwa Jumuiya, na alikuwa anajitambulisha kuwa Mwahmadiyya kwa kujivunia kabisa. Khalifa Mtukufu atba aliomba kuwa Mwenyezi Mungu Amtendee kwa ghofira na rehema na Awawezeshe familia yake wakubali Jumuiya. Ameen.

Heshima na Thawabu kwa Waahmadiyya

Kutoka uk.10

mpaka jua likaanza kuzama na hakuna yeyote aliekuja. Hatimaye karibu ya jioni maaskari polisi wengi wakafika walikuwa wamebeba pingu pia na walipofika tu wakachoma mji wa wasumbufu. Wakiwashika wote, kila mmoja akatiwa pingu nao wakashtakiwa kwa kwenda kinyume na amri halali ya dola na kujaribu kupambana na vyombo vya dola, na hapo wao wakapata adhabu waliostahili.

Hivyo nasema kweli kweli kuwa hivyo ndivyo itakavyo kuwa hali ya wakataaji wakosefu wa zama hizi. Kila mtu atashikwa kutokana na makosa ya ulimi wake, kalamu yake na mikono yake. Mwenye masikio na asikie.

Ni heshima na fahari kwa Tanzania

Kutoka uk. 3

sana.

Kuna haja ya kuzungumza na Abdulrazak Gurnah, mwandishi mpole na mwenye heshima ili kazi zake ziweze kutafsiriwa katika Kiswahili. Na kwa kufanya hivyo huuwa ndege wawili kwa jiwe moja. Kwanza kuwapa fursa Watanzania kuyafahamau aliyoyaandika Abdulrazak Gurnah lakini pia kuendeleza lugha ya Kiswahili ambayo inaendelea kujizolea umaarufu kila kukicha.

Kutokana na ushindi huu wa Abdulrazak Gurnah daima tukumbuke ukiona vyaelea vimuendwa. Tuzo hii imekumbusha mazuri yaliyokuwa yakifanyika mashuleni. Palikuwepo na majarida ya shule, vilabu vya uandishi, maktaba zilizosheheni fasihi anuai, michezo ya maigizo iliyoandikwa na wanafunzi wenyewe na kuigizwa n.k. Ni wakati sasa iundwe mikakati ya makusudi kabisa na ya kudumu kwa ajili ya kukuza vipaji na kuhuisha pendo la sanaa hii adhim. Kuna haja ya kuanzisha tuzo kwa ajili ya waandishi wetu wa lugha zote mbili za Kiswahili na Kiingereza ili waweze kukuza vipaji vyao na hatimaye kuipatia sifa nchi yetu.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

MUHAR - SAFAR 1443 AH | SEPTEMBA 2021 | IKHA 1400 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu^{saw}

Mtume^{saw}. alisema, Mwenye kumwangalia mjane na maskini atapata thawabu ya Haji na Jihadi **(Bukhari, Muslim).**

Makhalifa Walioongoka - Hadhrat Umar ibn Al-Khattab^{ra}

Katika hotuba ya Ijumaa iliyotolewa katika Jalsa Salana ya Uingereza tarehe 24/09/2021; Baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu V, Hazrat Amir ul Momeniin, Mirza Masroor Ahmad^{atba} ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz') alisema kwamba ataendelea kuangazia matukio kutoka maisha ya Hadhrat Umar (ra).

Ushindi Wa Baitul Maqdas (15 Hijria):

Khalifa Mtukufu^{atba}alisema kuwa chini ya uongozi wa Hadhrat Amr Bin Al-Aas^{ra} jeshi la Waislamu lilizingira Baitul Maqdas yaani Jerusalemu. Wakristo mwishowe walikubali kufanya suluhu, lakini wakaongeza sharti hili kuwa wanataka Hadhrat Umar Bin Al Khattab^{ra} aje mwenyewe na afanye suluhu. Kwa hivyo, Hadhrat Umar^{ra} baada ya kushauriana na masahaba^{ra} akaamua kwenda Baitul Maqdas.

Khalifa Mtukufu^{atba}alieleza maelezo ya wanahistoria mbalimbali kuhusiana na tukio hili na maoni yao mbalimbali kuyahusu matukio hayo.

Imesimuliwa kuwa Hadhrat Umar^{ra} alikuwa amekwisha ondoka tayari kuelekea Baitul Maqdas kabla ya kuwekwa sharti hili na wakazi wa Baitul Maqdas, kwa vile Hadhrat Amr Bin Al-Aas^{ra} alikuwa amemwandikia barua ya kuomba msaada. Hivyo, Hadhrat Umar^{ra} alikuwa ameisha



Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

ondoka tayari na alipokuwa njiani akasimama sehemu fulani iitwayo Jabiyah ambapo Hadhrat Umar^{ra} alikuwa anataka kushauriana na viongozi wa jeshi la Wasilamu. Katika sehemu hiyo Hadhrat Umar^{ra} alipata habari za sharti hili la kufanya suluhu na wakazi wa Baitul Maqdas.

Katika eneo la Jabiyah jemedari wa Jeshi la Waislamu walipokuja kwa kukutana na Hadhrat Umar^{ra} sawa na mwito wake. Hadhrat Umar^{ra} akawaona wakivaa mavazi yenye fahari sana ya wakazi wa Syria. Jambo hili likamchukiza sana Hadhrat Umar^{ra} lakini alipoambiwa na hao majemedari kuwa chini ya hayo mavazi, wao wamevaa deraya na wamevaa mavazi haya ili kupatana na wenyeji tu. Basi Hadhrat Umar^{ra} akakubali kauli yao.

Waislamu Wakafanya Mapatano na Wakristo Katika Jabiyah:

Khalifa Mtukufu^{atba}alisema kuwa Jabiyah ndiyo mahali ilipofanywa suluhu baina ya Waislamu na Wakristo. Wakristo walipokuwa wanakuja, walikuwa wamepanda farasi wao, na panga zao zilikuwa mikononi mwao zikawa zinametameta. Hapo, Waislamu pia wakatoa silaha zao, lakini Hadhrat Umar^{ra} akawaambia kuwa rudisheni silaha zenu maana hao Wakristo wamekuja kufanya suluhu ya amani. Ndani ya suluhu Hadhrat Umar^{ra} alisema kuwa wakazi wa Eliyah (Mahala ambapo Baitul Maqdas ilikuwa inapatikana) hawatadhuriwa, na nyumba zao na makanisa yao hayataharibiwa. Wale wanaotaka kurudi kwa Warumi wanaruhusiwa, na wale wanaotaka kuishi katika maeneo yao wako huru kufanya hivyo, maadamu wanalipa Jizyah (ushuru).

Khalifa Mtukufu^{atba}alisema kuwa masharti haya ya suluhu yanathibitisha waziwazi kuwa Waislamu hawakulazimisha watu kujiunga na dini yao, wakatetea uhuru wa kuabudu, na hawakumlazimisha mtu yeyote yule kutoa Jizyah, kila mtu aliruhusiwa kuwa ama aende mahali popote pengine, au atoe Jizyah.

Khalifa Mtukufu^{atba}alisema kuwa

Endelea uk 11



KITABU

Masomo ya Dini

Hii ni tafsiri ya Kiswahili ya *Religious Knowledge*.

Kimeandikwa katika mtindo wa swali na jibu, kitabu hiki kidogo lakini kilichosheheni kinajaribu kuweka wazi maelezo ya msingi ya imani ya Waislamu Waahmadiyya na desturi zake.

Pia kinatoa taarifa kuhusu Ahmadiyyat katika Afrika Mashariki.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba ya Tsh· 3,500/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com